## WMA YA MAKAME

Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Makame lipo kusini mwa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire. Eneo lina ukubwa wa kilometa za mraba 3719 zenye mapori ya wazi, uoto wa miiba na vichaka. WMA ya Makame ilisajiliwa mwaka 2009, lakini haikuanzinshwa rasmi mpaka mwaka 2002 ilipopokea haki ya matumizi. Jumuiya inaundwa na vijiji vitano vya Irkiushoibor, Makame, Katikati, Ndedo na Ngabolo venye takribani wakazi 10,000. Wakazi wengi katika vijiji hivi ni kutoka jamii ya wafugaji wa Kimasai. Vitalu vya uwindaji vya serikali vimekuwepo katika eneo hilo kwa miongo kadhaa. Mwaka 2014, Jumuiya iliingia katika mikataba wa kibiashara na kampuni mbili za uwindaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye biashara ya uwindaji wa kitalii katika WMA ya Makame. Juimuiya ilianza kupata mapato yake kutokana na mikataba hiyo wakati mradi wa utafiti wa PIMA ukielekea ukingoni.

## Kuhusu Mradi wa Utafiti wa PIMA

Utafiti wa faida na athari za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) kwa mazingira na umaskini (PIMA) ni mradi wa utafiti wa kimataifa ulioendeshwa kwa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha London, Chuo Kikuu cha Kopenihageni, Chuo Kikuu cha Imperial London, Chuo Kikuu cha Edinburgh, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Ufuatiliaji wa Uhifadhi Duniani, na Jumuiko la Maliasili Tanzania. PIMA ilikusanya taarifa za ngazi ya kaya kuhusu mali na hali za kimaisha kwa kutumia madodoso na kwa kuzipanga kaya katika madaraja tofauti ya kipato. PIMA pia ilikusanya taarifa katika ngazi ya kijiji na WMA kuhusu uendeshaji wa WMA ikiwa ni pamoja na ugawanaji mapato. Taarifa hizi zilikusanywa katika vijiji 42 ndani na nje ya WMA sita zilizopo kaskazini na kusini mwa Tanzania. Upangaji wa kaya katika madaraja ya kipato ulifanyika kwa kaya zaidi ya 13,500. Dodoso lilitumika kukusanya taarifa kuhusu mali na mbinu za kujikimu kabla na baada ya kuanzishwa kwa WMA kutoka kwa wanaume na wanawake katika kaya zinazokaribia 2,000 (lengo ni kulinganisha hali ya maisha kati ya kipindi cha mwaka 2014-15 wakati wa utafiti wa PIMA na hali ilivyokuwa mwaka 2007 kulingana na kumbukumbu ya mhojiwa). Kwa kulinganisha mabadiliko ya hali ya maisha kabla na baada ya WMA kati ya vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA, athari za WMA kwa hali ya maisha zinaweza kujulikana (Kielelezo 2).

## Mapato ya WMA ya Makame

- Mapato yatakanayo na tozo mbalimbali katika WMA yanapaswa kugagwanywa kulingana na Kanuni zinazosimamia Maeneo ya Jumuiya ya Wanyamapori za mwaka 2008 na 2012 (Kielelezo Na. 3).
- Mgawo wa mapato ya utalii hutolewa kwa serikali kuu (*nyeusi*) na kwa halmashauri ya wilaya *(nyeupe)*
- Mapato yanayobaki hurudishwa kwa Jumuiya inayosimamia WMA ambayo inaweza kubakiza nusu ya mapato *(michirizi)* na kugawanya nusu nyingine kwa vijiji wanachama (kijivu mpauko)
- Jumuiya ya Makame ilianza kupata mapato mwishoni mwa mwaka 2013 ambayo yalifikia dola za kimarekani 15,000
- Mpaka wakati taarifa hii inaandaliwa, hakukuwa na taarifa kuhusu mgawanyo wa pesa hizo.

## Ramani ya WMA ya Makame




**Kielelezo Na 1: Ramani ya Makame WMA (sehemu nyeupe). Imeandaliwa na J. Bluwstein.**

## Jedwali la taarifa Muhimu: WMA ya Makame

| | |
|---|---|
| Wilaya | Kiteto |
| Vijiji Wanachama | 5 |
| Idadi ya Wakazi | 9,751 |
| Eneo | 3,719 km$^2$ |
| Mwaka wa usajili | 2009 |
| Jina la asasi ya kiraia | Indema |




**Kielelezo Na. 2: Mbinu iliyotumiwa na PIMA kuonesha mabadiliko yaliyosababishwa na WMA**




**Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa mapato kutoka na ada za uwindaji wa kitalii na utalii wa picha kulingana na Kanuni za Utalii wa Picha 2008 na Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Wanayapori za mwaka 2012.**

* WMA inaweza kufanya makubaliano ya kuongeza kiwango cha ada, ambapo 100% ya kiwango cha ziada hubakia kwa WMA. ** Ada kubwa kabisa kwa nyara hutozwa kwa aajili ya uwindaji wa Tembo: Kati ya dola za kimarekani 10,000 - 25,000, kutegemea na ukubwa wa meno ya Tembo. *** Hukusanywa na serikali kuu, na baadae kugawanywa kwa WMA baada ya kukatwa kodi. Ada hizi ni pamoja na ada ya mikataba, ada ya kulaza wageni, ada ya kutembea eneo la WMA, ada ya kuingiza gari n.k.

## Mabadiliko ya Hali ya Maisha katika WMA ya Makame

### Mali

- Kulingana na mitazamo ya wakazi, kaya za Makame zilipangwa katika makundi ya 'maskini sana' 'maskini' 'kawaida' na 'tajiri' kufuatana na kiwango cha mali kwa mwaka 2014 na kumbukumbu za umiliki mali kwa mwaka 2007
- Kaya nyingi zilikokuwa 'tajiri' mwaka 2007 ziliendelea kubakia 'tajiri' mwaka 2014 (kwa vijiji vya WMA na visivyo kwenye mpango wa WMA)
- Kwa wastani, ni kaya chache katika vijiji vya WMA ziliweza kuongeza mali zao kati ya mwaka 2007-2014 kuzidi kaya katika vijiji visivyo vya WMA (Kielelezo Na. 4)
- Kati ya 2007-2014, umasikini uliongezeka kwa kaya chache katika vijiji vya WMA kuliko katika vijiji visivyo kwenye WMA. Kaya zilizokuwa 'maskini sana' mwaka 2007 ziliongeza umiliki wa mali mwaka 2014 katika vijiji vya WMA zaidi ya vijiji visivyokuwa kwenye WMA (Kielelezo Na. 4)
- Hata hivyo, tofauti ya mabadiliko kati ya vijiji vya WMA na vile visivyo kwenye WMA kabla na baada ya WMA yanaweza kuwa hayatokani na WMA kwa sababu mapato ya WMA yameanza kupatika hivi karibuni.




**Kielelezo Na. 4: Mabadiliko ya hali ya maisha kati ya mwaka 2007 na 2014 kwa kaya zilizoko kwenye vijiji vya WMA na nje ya WMA. Kwa kila kaya 10, takribani kaya 3.5 zimekuwa tajiri zaidi na 1 maskini zaidi kwa maeneo yasiyo ya WMA. Katika maeneo ya WMA, takribani kaya 2.5 kati ya 10 zimekuwa tajiri zaidi, na 0.5 zimekuwa maskini zaidi baada ya kuanzishwa kwa WMA.**

### Upatikanaji wa Maliasili na Mapato yatokanayo na Mazingira

- Katika utafiti huu, upatikanaji wa maliasili maana yake ni kiwango ambacho sheria na kanuni huzuia au husaidia kaya kupata kuni, fito, asali ya porini, vyakula vya porini n.k. kwa ajili ya matumizi au biashara.
- Mapato yatokanayo na mazingira imaaminisha mapato yatokanayo na ukusanyaji na/au uuzaji wa maliasili.
- Katika vijiji ya WMA na vile visivyo vya WMA, mapato yatokanayo na kuni yameongezeka kulinganisha na maliasili nyingine (Kilelelezo Na. 5). Mapato yatokanayo na nguzo/fito/nyasi kwa ajili ya ujenzi na asali ya porini yamepungua
- Wakazi waliohojiwa kwa ajili ya utafiti huu hawakutaja mbao na mkaa kama sehemu ya matumizi ya msitu. Kielelezo Na. 5 hakioneshi matumizi hayo.
- Upatikanaji wa bidhaa nyingi zitokanazo na mazingira katika WMA ya Makame haujabadilika, ingawa baadhi ya wakazi wanafikiri upatikanaji wa asali ya porini umekuwa wa shida.




**Kielelezo Na. 5: Mapato yatokanayo na bidhaa za mazingira kwa vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2007 na 2014.**

### Mbinu za Kujikimu Kimaisha

- Mapato yatokanayo na shughuli zinazoegemea katika mazingira (Kilimo, ufugaji na mazao ya porini) yanachangia aslimia 72 ya mapato yote ya kaya za Makame kwa mwaka 2014 na asilimia 77 kwa kaya zisizo za WMA (Kielelezo Na. 6). Mazao ya porini yanajumuisha kuni, vifaa vya ujenzi, mbao, samaki, asali n.k.
- Mchango wa mapato ya kilimo, ufugaji na mazao ya porini kutoka 2007 hadi 2014 umepungua kwa vijiji WMA na vile visivyo vya WMA (kielelezo Na. 7)
- Vijiji vya WMA viliongeza utegemezi katika mapato yatokanayo na kazi za kibarua, biashara na misaada kutoka kwa ndugu waishio mijini kuanzia mwaka 2007 hadi 2014. Mapato yatokanayo na biashara yalipungua katika vijiji visivyo vya WMA (kielelezo Na. 7)




**Kielelezo Na. 6: Mchango (kwa asilimia) wa vyanzo mbalimbali kwenye pato la jumla (mzunguko mzima) katika vijiji vya WMA ya Makame na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2014**




**Kielelezo Na. 7: Mabadiliko ya mchango wa chanzo cha mapato kwa mwaka 2007-2014 kwa vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA**

## Ardhi ya Kilimo

- Ardhi ya kilimo inapimwa kwa kulinganisha uwiano wa idadi na umri wa wanakaya, na inaripotiwa kwa kufuata uwiano wa ukubwa wa eneo na idadi ya watu wazima katika kaya i.e. 'adult equivalent' (AE)[1]
- Kufutia uwiano wa ukubwa wa eneo kwa mtu mzima, wakazi wa vijiji vya WMA wana ardhi pungufu ya kilimo kuliko wenzao wa vijiji visivyo vya WMA (WMA: eka 1/mtu mzima, vijiji visivyo vya WMA: eka 1.5/mtu mzima).
- Kwa mwaka 2014 watu wengi wanamiliki ardhi ya kilimo ambayo ni pungufu ukilinganisha na mwaka 2007. Kupungua kwa umiliki wa ardhi ya kilimo katika vijiji visivyo vya WMA kunazidi vijiji vya WMA.
- Kwa zaidi ya kipindi cha miaka 10 iliyopita, watu kutoka vijijiji na wilaya nyingine wamehamia katika vijiji vya WMA ya Makame na kuanzisha mashamba katika eneo la WMA kwa kuwa sheria za WMA zilikuwa hazisimamiwi au kufuatwa. Kuna uwezakano mkubwa kuwa mashamba haya hayakupewa vibali wala kurasimishwa.
- Wakazi wengi wa Kimaasai wanapinga ubadilishaji wa ardhi yao ya malisho ya mifugo kuwa maeneo ya kilimo kunakofanywa wahamiaji. Kwa wafugaji hao, WMA ni njia ya kuwaondoa wakulima waliohamia na kuzuia maeneo muhimu ya malisho hayabadilishiwi kuwa mashamba.

## Ardhi ya Malisho

- Wakazi wengi wa Makame ni wafugaji. Kwa hiyo ardhi ya malisho ni muhimu sana katika maisha yao
- Uchungaji katika WMA ya Makame kwa sasa unaruhusiwa katika majira yote na hakujakuwa na mabadiliko ya upatikanaji wa malisho katika vijiji vya Makame tangu mwaka 2007

## Mifugo

- Neno 'mifugo' linamaanisha wanyama wote wafugwao majumbani. Ili kurahisisha kulinganisha aina tofauti za wanyama na idadi (kama vile mbuzi, ndama na ng'ombe), PIMA inatumia kipimo kijulikancho kama 'kipimo cha mifugo'[2]
- Kaya katika vijiji vya WMA zinamiliki mifugo michache mwaka 2014 kuliko mwaka 2007 (Kielelezo Na. 8). Kaya katika vijiji nje ya WMA wanamiliki mifugo mingi zaidi mwaka 2014 kulinganisha na mwaka 2007
- Kwa Makame, sababu ilityotajwa zaidi kuelezea kupungua kwa mifugo ni magonjwa na mahitaji ya fedha.




**Kielelezo Na. 8: Mabadiliko ya idadi ya mifugo inayomilikiwa na kaya katika vijini vya WMA ya Makame kati ya mwaka 2007 na 2014 kwa kutumia 'kipimo cha mifugo' (hapa ikioneshwa kama ng'ombe)**

## Athari za Wanyamapori kwa Wakazi wa vijiji vinavyounda WMA ya Makame

- Athari za wanayamapori kwa wakazi ni pamoja na vifo na majeraha kwa binadamu na mifugo, uharibifu wa mazao na mali nyingine. Matukio haya husababisha hasara kubwa.
- Kaya 7 kati ya 10 za vijiji vya WMA zilipata athari za kuharibiwa mazao yao katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ukilinganisha na kaya 5 kati ya 10 za vijiji visivyo vya WMA (Kielelezo Na. 9)




**Kielelezo Na. 9: Wastani wa idadi ya kaya katika vijiji vya WMA (70%) na visivyo WMA (50%) ambazo zimekumbwa uharibifu wa mazao kutokana na uvamizi wa wanyamapori katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti.**

- Kaya katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA zimetaja kutokuwepo mabadiliko ya viwango vya uharibifu wa mazao kati ya mwaka 2007 na 2014.
- Katika WMA ya Makame, kijiji cha Irkiushoibor kiliripoti kiwango kikubwa cha uharibifu wa mazao ambapo kaya 9 kati ya 10 zimeripoti kuathirika.
- Ingawa kwa wastani kiwango kikubwa cha kaya za WMA zilipata madhara ya uharibifu wa mazao (Kielelezo Na. 9), hasara kwenye kaya katika vijiji visivyo vya WMA ni kubwa zaidi (Kielelezo Na. 10)
- Tatizo la wanyamapori wakali kushambulia mifugo ni kubwa katika WMA ya Makame
- Kiwango cha mifugo inayoliwa na wanayamapori wakali ni sawa kwa vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA.
- Katika WMA ya Makame WMA, vijiji vya Ndedo na Ngabolo viliripoti idadi kubwa zaidi ya mifugo kuliwa na wanayamapori wakali.
- Katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA uvamizi wanyamapori wa wanyamapori wakali kwa mifugo unasababisha hasara ya wastani wa mnyama (mfugo) mmoja kwa kipimo kimoja cha mfugo kwa matukio ya hivi karibuni.




**Kielelezo Na. 10: Wastani wa hasara iliyotokana na uharibifu wa mazao kwa kaya katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA. Angalizo: Kiwango cha hasara kimekokotolewa kutokana na makadirio ya eneo lililoharibiwa, uzalishaji wa mazao, na makadirio ya pesa za mauzo ya mazao**

## Hitimisho

Matokeo ya utafiti huu hayaoneshi kwa uhakika athari za WMA kwa mabadiliko ya hali ya maisha katika vijiji vya WMA Makame na vile visivyo vya WMA. Mabadiliko katika umiliki mali, shughuli za kujikimu kimaisha, umiliki wa ardhi pamoja na mifugo ni sawa kwa makundi yote mawili ya vijiji. Utofauti katika athari za uharibifu wa wanyamapori hauoneshi mwenendo malaamu. Hata hivyo, sheria za WMA zimeanza kusimamiwa hivi karibuni (mwaka 2015) na mapato ya WMA yameanza kupatikana hivi karibuni (mwaka 2014). Kwa hivyo basi, kukosekana kwa utofauti kati ya kaya za WMA na zile zisizo za WMA si jambo la kushangaza kwa sasa. Hali hii inaweza kubadilika baada ya sheria za WMA kutekelezwa kwa miaka kadhaa.



Kielelezo Na. 11: Picha na J. Bluwstein

WMA ya Makame ni WMA pekee katika utafiti wa PIMA ambayo kwa kiasi kikubwa wakazi wake wameonekana kuunga mkono wazo la kutenga sehemu ya ardhi ya kijiji kwa ajili ya hifadhi ya wanyamapori. Wakazi hao ambao wengi hujihusisha na kilimo na ufugaji wanaamini kuwa WMA inaweza kulinda ardhi yao kwa ajili ya malisho dhidi ya uwezekano wa upanuzi wa Pori la Akiba la Mkungunero (na kuathiri vijiji vya Irkiushoibor na Katikati ), na dhidi ya wakulima wahamiaji. WMA pia inaweza kuwaathiri wakazi wa Makame waonataka kupanua shughuli zao za kilimo. Shuguli zinazoegemea mazingira (kilimo, ufugaji, mazao ya porini) zinachangia asilimia 72 ya jumla ya mapato ya kaya za Makame kwa mwaka 2014. Hivyo, kuendelea kuwepo kwa upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji na mazao mengine ya porini kama vile kuni na vifaa vya ujenzi ni muhimu kwa wakazi Makame.

Kunaweza kuwa na faida au athari nyingine za WMA zaidi ya zile zilizoanishwa na utafiti wa PIMA. Migogoro ya matumizi ya ardhi kwa ajili malisho ya mifugo dhidi ya kilimo katika maeneo ya WMA ya Makame imepelekea wilaya kutishia kuwafukuza wakulima. Tishio hilo limesababisha wakulima kuondoka kwa hiari. Zaidi ya hayo, WMA ilianza kufanya kazi wakati utafiti wa PIMA unafikia ukingoni. Kwa hiyo matokeo yatokanayo na Mapato ya WMA hayawezi kuonekana katika utafiti huu .

## Kumbumbuku Rejea

[1]Katika matokeo haya, ardhi ya kilimo imeainishwa na idadi ya watu katika kaya, jinsia na umri, kwa sababu wanaume, wanawake, na watoto wa umri tofauti huhitaji kiwango tofauti cha chakula, na hivyo ukubwa sawa wa ardhi humaanisha uwezo tofauti wa kutosheleza mahitaji kwa kaya mbalimbali. Kwa kutumia mfumo sanifu, tunawajumlisha wanakaya na kuwaweka katika kipimo cha ‘uwiano wa mtu mzima’ (AE), ambacho ni rahisi kulinganisha umiliki wa ardhi ya kilimo na mahitaji kwa kaya.

[2]Kama ambavyo PIMA imetumia mfumo sanifu wa uwiano wa mtu mzima (AE), tunatumia 'kipimo cha mifugo' ili iwe rahisi kulinganisha makundi ya mifugo yanayoundwa kwa aina na ukubwa tofauti wa mifugo na mahitaji yao tofauti ya chakula. Kipimo kimoja cha mfugo ni sawa na ng’ombe mmoja mkubwa wa kilo 250kg. Mbuzi au kondoo kwa mfano, anahesabiwa kuwa sawa na moja ya kumi ya ng'ombe.

## Shukrani

PIMA inawashukuru wakazi wa vijiji vya Irkiushoibor, Makame, Ndedo-Ndedo, Ndedo-Ngabolo, Katikati, Kimotorok, Namalulu na Gidemar, na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Makame kwa kushiriki katika utafiti huu. Mradi wa utafiti wa PIMA umefadhiliwa na ESPA: Mpango wa Utafiti wa Mazingira na Kuondoa Umaskini. ESPA inaendeshwa kwa pamoja na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Baraza la utafiti wa Mazingira (NERC) na Baraza la Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRC). Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti hii: www.ucl.ac.uk/pima

Jarida hili limeandaliwa na S. Funk kutokana na takwimu zilizokusanywa na mradi wa utafiti wa PIMA. A. Keane, M. Reinhardt Nielsen, J. Friis Lund, J. Bluwstein and K. Homewood kwa pamoja waliandaa mbinu za kukusanya, kuchambua na kutafsiri takwimu za PIMA. J. Olila aliongoza kikundi cha wakusanya takwimu. M. Msuha and N. Burgess walihusika na takwimu za wanyamapori.

## Marejeo

WWF (2014): Tanzania's Wildlife Management Areas, 2012 Status Report.

**Mawasiliano:** K. Homewood, Chuo Kikuu cha London, Idara ya Anthropologia. k.homewood@ucl.ac.uk